

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NNE

KIKAO CHA NANE

09 SEPTEMBER, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NNE

KIKAO CHA NANE – TAREHE 09 SEPTEMBER, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Maelezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*Agreement Establishing African Continental Free Trade Area – AfCFTA*).

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*Agreement Establishing African Continental Free Trade Area – AfCFTA*).

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

95. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Shule ya Sekondari ya Kidato cha Tano na Sita Mungaa ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa kipindi cha Kampeni Mwaka 2020 alipopita Jimbo la Singida Mashariki.

96. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara zinazopanda milimani Arumeru Mashariki ili kuwafikishia Wananchi huduma pamoja na kupunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara kwa barabara

hizo ambapo gharama zake ni kubwa kutokana na ugumu wa kijiografia.

97. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO (BABATI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka kati ya Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu na Vijiji vya Olacity na Minjingu.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

98. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhuisha vigezo vya mfumo wa miradi ya kimkakati kupitia maandiko ya miradi ili iweze kusaidia Halmashauri kubuni miradi ya kiuchumi.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

99. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali haioni haja ya kutenga fedha za kuvunja Mlima Londo ili kuunganisha Wilaya ya Malinyi na Namtumbo hata kwa kiwango cha changarawe ili njia hii iweze kupitika huku Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Namtumbo Lumecha Km 296.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

100. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu usalama wa Askari ambao wakati mwingine huvamiwa

na kujeruhiwa pamoja na kuporwa silaha wakati wakiwa kazini.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

101. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

- Je, Serikali ina mikakati gani ya ziada ya
- kudhibiti tatizo la utapeli na wizi wa kimtandao kupitia simu za mkononi.

WIZARA YA MAJI:

102. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itachimba visima vya maji katika Kata ya Mwamanyili Kijiji cha Milambi Wilayani Busega ili kuwapunguzia adha ya maji Akina Mama wa Kijiji hicho.

WIZARA YA NISHATI:

103. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Mradi wa Umeme wa Ujazilizi katika Mkoa wa Manyara na Jimbo la Mbulu Vijijini ili kuwafikia Wananchi wengi ambao hawakupitiwa na Mradi wa REA I, II na III.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

104. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvuna Mamba katika Mto Ruvu hasa katika Vijiji vya Kigamila, Bwila Juu, Magogoni, Bwila Chini, Kongwa, Tulo, Lukuhinge, Kata za Mvuha na Serembala katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini ili kupunguza vifo vinavyosababishwa na Mamba hao.

V. HOJA ZA SERIKALI:

MAAZIMIO:

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Azimio la Bunge la kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (*Agreement Establishing African Continental Free Trade Area – AfCFTA*).



**DODOMA
09 SEPTEMBER, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**